# FORM 4 EVALUATION TEST 2021
# KISWAHILI PAPER 3

SEHEMU A USHAIRI

1. LAZIMA:

Kila nikaapo hushika tama
Na kuliwazia hali inayonizunguka.
Huyawazia madhila
Huziwazia shida
Huiwazia dhiki
Dhiki ya ulezi
Shida ya kudhalilishwa kazini
Madhila ya kufanyiwa dharau
Kwa sababu ya jinsia yangu ya kike.

Hukaa na kujidadisi
Hujidadisi kujua kwa nini
  Jamii haikisikii kilio change
  Wezangu hawanishiki mikono
Bali wananidharau kwa kuukosoa utamaduni

Hukaa na kuhiuliza
I wapi afua yangu dunia hii
I wapi raha yangu ulimwengu huu
I wapi jamaa nzima ya wanawake?

Maswali

1. Shairi ulilosoma ni la aina gani? (alama 2)
2. Toa anwani faafu ya shairi (alama 2)
3. Eleza dhamira na maudhui ya shairi(alama 3)
4. Taja na ueleze tamathali tatu za fani ambazo zimetumiwa katika shairi hili.(alama 6)
5. Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari.(alama 4)

**SEHEMU YA B**

KEN WALIBORA, KIDAGAA KIMEMWOZEA

2. Jibu swali la 2 au la 3

   Kidagaa kimemwozea ni Anwani mwafaka ya riwaya ya'' kidagaa kimemwozea''Eleza(alama 20)

3. " hata haramu huhalalishwa ati…..Hutegemea mtendaji ni nani na mtendwa ni nani."
   (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili.(alama 4)
   (b) Eleza tamathali kuu katika maneno ya swali.(alama 2)
   (c) Thibitisha ukweli unaotokeza katika dondoo.(alama 6)
   (d) Eleza sifa za wahusika wafuatao

      Imani

      D.J (alama 8)

**SEHEMU C TAMTHILIA**

TIMOTHY AREGE: MSTAHIKI MEYA

JIBU SWALI LA 4 AU 5

4. .Si nyingi nd'o mjuao…….! Mimi sifahamu ila nikiona afadhali.
   a. Fafanua muktadha wa dondoo hili.(alama 4)
   b. Fafanua maisha ya msemaji.(alama I0)
   c. Taja tamathali iliyotumiwa katika dondoo hili.(alama 2)
   d. Kwa undani, fafanua maudhui yanayoendelezwa na msemaji.(alama 4)
5. Kupitia mifano, eleza mbinu zozote kumi zilzioendelezwa na utawala wa Sosi ambao ni utawala Dhalimu.(alama 20)

**SEHEMU YA D**

**DAMU NYESUSI NA HADITHI NYINGINE –KEN WALIBORA NA S.A MOHAMED.**

**JIBU SWALI LA SITA AU LA SABA**

6. GILASI YA MWISHO MAKABURINI (S.A MOHAMED )

   "una nini Msoi? Ama kweli itikadi na ushirikina vimekudhibiti kweli kweli.

   (i) Eleza muktadha wa dondoo hili.

   (ii) Eleza maudhui makuu ya hadithi (alama 16)
7. Ndoa ya samani: Omar Babu(Abu marjan)

   Ukirejelea hadithi ya Ndoa ya Samani jadili maudhui ya Ndoa, <u>mali</u> na <u>mapenzi</u>.(alama 20)

**SEHEMU E**

**FASIHI SIMULIZI**

a) Eleza sifa za malumbano ya utani katika jamii.(alama 10)

b) (i) nyiso ni nini?(alama 2)

(ii) eleza sifa nne za nyiso.(alama 8)